# Wasanii wa Sauti za Busara 2011

## AFRICAN STARS BAND (AKA TWANGA PEPETA) (Tanzania)

**Jumapili 13, saa 6:25 usiku Old Fort**
**Mtindo**: band, dance, rumba

Ni miongoni mwa bendi liiyo na wapenzi wengi sana,inatambulika Tanzania kama Twanga pepeta kutokana na mtindo wake wa kiuchezaji. Wameshafanikiwa kupata tunzo nyingi tangu ilipoanzishwa mnamo mwaka 1994. Ilishapata tuzo ya kuwa bendi bora ya mwaka, tuzo ya uchezaji bora na bendi bora ya mziki wa dance na wameshafanikiwa kutoa santuri nane zikiwemo za kusikiliza na kuona na nyimbo nyingi kati ya hizo zimefanikiwa sana mpaka kupata tuzo za mwimbo bora, kama mwimbo wa *Mtu Pesa*. Bendi inachanganya mitindo tofauti kama Rhumba, Ndombolo, Blues, Chacha, Zouk na hata Soca. Katika tamasha la mwaka 2011 la Sauti za Busara Twanga Pepeta watapandisha stejini watu 17 kati ya 40 ambao ni wanachama wa kundi. Bendi nzima itashusha burudani na kutoa show ya kukata na shoka siku ya mwisho ya kufunga tamasha.

www.africanstars.net

**Albam:**
Kisa cha Mpemba (1999); Jirani (2000); Fainalu Uzeeni (2001); Chuki Binafsi (2002); Ukubwa Jiwe (2003); Mtu Pesa (2004); Safari (2005)

---

## ATEMI & THE MA3 BAND (Kenya)

**Jumapili 13, saa 2:20 usiku Old Fort**
**Mtindo**: band, fusion, pop

Carol Atemi Oyungu ni mmoja kati ya waimbaji machachari katika ukanda wa Africa Mashariki. Mwaka 2003 alijiunga na kundi maarufu la Eric Wainaina, alikuwa akiimba sauti ya pili. Atemi pamoja na Erik na Mapinduzi Band wameshafanya maonyesho ndani ya Afrika na Ulaya na hata katika tamasha la Sauti za Busara mwaka 2008. Alifanikiwa kutoa mwimbo wake wa kwanza mwaka 2004 huku akiendelea kufanya maandalizi ya albam yake ya kwanza na mwaka 2008 inaitwa *Hatimaye*. Sasa anaendelea kufanya maandalizi ya albam yake ya pili kama solo albam ambayo inakaribia katoka mwaka 2011. Atemi anatumia mchanganyiko wa (neo-soul na afro-soul). Sauti ya Atemi imekuwa ikifananishwa na ya Mariam Makeba. Mwaka huu Atemi anarudi tena kwenye tamasha la Sauti za Busara na Ma3 Band.

www.gatwitch.com
www.myspace.com/atemidiva

**Albam**:
Hatimaye (2008)

Shukran kwa Fly540

## BISMILLAHI GARGAR (Kenya)

**Ijumaa 11, saa 2:20 usiku Old Fort**
**Mtindo**: fusion, roots, traditional

Bismallah Gargar ni mchanganyiko wa wanawake wenye asili ya Somalia kutoka Garisa kaskazini mashariki mwa Kenya. Jina la Bismillah linatokana na neno la kisomali lenye maana ya “kwa jina la mungu” (in the name of god) na “gargar” ina maana ya kuwaweka watu pamoja (bringing people together). Kundi lilianzishwa mwaka 2003 lengo la kundi lilikuwa ni kujiwezesha kutokana na baadhi ya sehemu kulikuwa kuna mila potofu za kumkandamiza mwanamke. Albam yao ya kwanza waliipa jina la *Garisa Express* iliyorekodiwa kwa muda wa miaka miwili ilipitia safari ndefu sana kwenda na kurudi kati ya Garisa na Nairobi. Muziki wao ni wa kiasili na wa kipekee wenye lugha ya kisomali. Bismillahi Gargar walirekodi na vyombo vya kisasa na kuwafanya albam yao ya *Garisa Express* kuwa ya kujivunia kwa mwaka 2010 nchini Kenya.

**Albam**:
Garissa Express (2010)

Shukran kwa Fly540

---

## BLICK BASSY (Cameroon)

**Ijumaa 11, saa 3:20 usiku Old Fort**
**Jumapili 13, saa 3:10 usiku Old Fort**
**Mtindo**: band, fusion, jazz, roots

Blick Bassy ni sauti ya kinafsi (soul) ya Cameroon - nafsi kwa maana ya kwamba sauti anayoimba hutokea ndani ya roho. Katika albamu yake ya hivi karibuni mwimbaji, mtunzi, mpiga gitaa na mpiga tumba ameuchukua muziki wa Afrika ya kati na Afrika Magharibi na kuuchanganya na mtindo ya Bossa nova, jazz na soul. Gitaa la Bassy huchezwa na kwa mtindo wa kiana ambao huwalevya mashabiki, sauti laini za waimbaji na utajiri wa kora vilevile ala za kiasili kama vibuyu na bass husababisha sauti ya kipekee, ambayo huleta miondoko ilio Groovy. Léman(2008) ni album yake ya kwanza iliorekodiwa katika studio za Salif Keita huko Bamako, Mali. Bassy kiongozi wa sasa anaishi Paris, Ufaransa. "Léman maana yake ni kioo” anaelezea Blick. Anaendelea “kioo ni huakisi jamii. Na unaweza pia kuona nyuma yenu kwa kutumia kioo.” Bassy alizaliwa mwaka 1974, pamoja na ndugu zake 10 katika mji mkuu wa Cameroon, Yaoundé. Akiwa na umri wa miaka 10, Bassy alipelekwa kuishi na babu yake kwa miaka miwili huko Mintaba, kijiji kidogo katikati ya Cameroon. Babu yake alimlea Bassy kwa desturi na utamaduni, na mafunzo ya aina mbalimbali ya kazi, kama vile uvuvi, uwindaji na kilimo. Vilevile alimfundisha elimu ya muziki. Huko Mintaba, wanakijiji hawapendelie kufanya mazungumzo mengi lakini zaidi hupendelea sana kuimba wakati kazi zao za kila siku. Mama yangu alikua akimba kuanzia asubuhi mpaka usiku. Yeye ni mmoja wa watu walionipa moto wa matarajio kimuziki na ndiye alienifundisha jinsi ya kuimba. “Nilianza kwa sikiliza wanamuziki kama Marvin Gaye, Gilberto Gil na Nat King Cole.” Nilitambua mapema kuanilitaka kuchanganya uzuri wa utamaduni wangu wa Bassa na mila zake za muziki na hivyo kuniwezesha kuujenga muziki wangu soulful". Tangu 2005 Bassy alipohamia Paris, kashafanya kazi na Manu Dibango, Cheikh Tidiane Seck, Lokua Kanza na Etienne Mbappé.

www.worldconnection.nl/wclayout/index.php?site_id=37

**Albam**:
Léman (2008)

Shukran kwa CULTURESFRANCE

## CHRISTINE SALEM (Reunion)

**Jumatano 9, saa 3:40 usiku Old Fort**
**Mtindo**: fusion, traditional, roots

Sauti ya "marogo" ya mwanadada Christine Salem inatusafirisha katika safari ya Muziki na kutuvusha bahari ya hindi nyimbo zake utilia mkazo na kutuelezea juu ya ugumu wa maisha mahangaiko katika lugha za creole, kimalagasy, kikomoro na Kiswahili za mababu zetu. Salem Tradition ni kundi kutoka kisiwa cha Reunion, huchanganya aina ya muziki sega, blues na maloya. Kama mtunzi na muimbaji mwenye umri mdogo katika kundi zima alianza kazi za sanaa mwaka 1997. Yeye huchanganya tamaduni za bahari ya hindi na mila na desturi za watu wa Reunion kwa kutumia vifaa vya kiafrika, kwenye maonyesho yake. Mwanamuziki huyu huonekana mwenye nguvu na hisia kali vilevile hucheza na watazamaji wake na kuteka hisia zao kasha kuproduce zaidi.

www.myspace.com/salemtradition

**Albam**:
Krié (2003); Fanm (2005); Lanbousir (2010)

Shukran kwa Direction Régionale des Affaires Culturelles, Conseil Régional, Département de la Réunion & Lundi Production

---

## CULTURE MUSICAL CLUB (ZANZIBAR)

**Ijumaa 11, saa 1:00 usiku Old Fort**
**Mtindo**: kidumbak, roots, taarab ya asilia

Kundi lilianzishwa mwaka 1958. Kundi hili hufanya maonyesho mengi katika matamasha ya Zanzibar. Mara nyingi kundi huwa linasafiri na vifaa vya steji na jenereta mpaka vijijni kwa ajili ya kuwapa watu wa huko burudani. Kundi limetoa nyimbo nyingi katika soko la ndani na nyimbo mitano katika soko la kimataifa. Kwa kawaida walikuwa wanapiga kidumbaki na taarab wanapokwenda bara la Ulaya tangu mwaka 1996, na katika miaka michache iliyopita wamefanya shoo ndani ya Marekani, Dominic Republic na Japan pia.

**Albam**:
Taarab 4: The Music of Zanzibar – Culture Musical Club (1988, GlobeStyle), Spices of Zanzibar (1996, Network), Kidumbak Kalcha: Ng 'ambo – The Other Side of Zanzibar (1997, Dizim), Bashraf – Taarab Instrumentals from Zanzibar (2000, Dizim), Waridi – Parfums de Zanzibar (2003, Jahazi), Zanzibar – De l'âme à la danse / Zanzibar – Soul & Rhythm (2003, Jahazi)

---

## DJAAKA (Mozambique)

**Jumamosi 12, 3:10 usiku Old Fort**
**Mtindo**: band, roots, traditional

Djaaka imeanzishwa mji wa Beira, katikati ya Mozambique mwaka 2001 wanapiga miziki ya aina mbalimbali kutoka Mozambique. Sauti ya Djaaka inatambulika hasa kutokana na kutumia sana ala ya marimba katika nyimbo zake nyingi. Djaaka ni muziki wa kisasa uliochanganywa na wa asili (funk na roots), wanamuziki wenye ujuzi na wachezaji mahili.

www.zammo.dk
www.myspace.com/djaaka

**Albam**:
Mbhole Mbolhe na Yona (2002); Unidade Nacional (2009)

## DJELI MOUSSA DIAWARA (Guinea)

**Jumapili 13, saa 4:15 usiku Old Fort**
**Mtindo**: fusion, jazz, roots

Mwimbaji na mtunzi Djeli Moussa Diawara ni miongoni mwa wawapigaji wakwanza ulimwengu wa kora. Kama kaka yake wa kambo yake Mory Kante – alifunzwa sanaa na wazazi wake. Huchanganya mitindo *flamenco*, *salsa*, na *jazz*. Ameshafanya rekodi na Ali Farka Toure, Carlos Santana, Bob Brozman, Manu Dibango, Janice de Rosa, Stephan Eicher.
www.djelimoussadiawara.com

**Albam**:
Yasimika (1983); Soubindoor (1988); Cimadan (1992); Sobindo (1996); Flamenkora (1998); Ocean Blues – from Africa to Hawai with Bob Brozman (2000); Sini (2006)

Shukran kwa Spedidam

---

## GROOVE LÉLÉ (Reunion)

**Alhamisi 10, saa 3:10 usiku Old Fort**
**Mtindo**: fusion, traditional

Groove Lele wamedhamiria kuueneza muziki wa gwiji la muziki wa maloya (babu) Julien Philean Gramoun Lele. Kundi lina wanamziki 12; kati yao wanne ni watoto wake. Muziki wa maloya ulianzishwa kwa siri katika kipindi cha utumwa na matatizo ya ukoo ndani ya Reunion. Hasa kwa kuzingatia sauti na vyombo vya muziki vya asili. Wakiwa stejini, uchezaji, uimbaji muziki vyote vilikuwa vinaelezea kilio cha uhuru, muziki huu kipindi cha biashara ya utumwa ulipigwa marufuku. Gramoun Lele katika kipindi cha maisha yake alishawahi kurekodi CD kadhaa za makabila ya *vaudou*. Muziki wenye mchanganyiko wa ushawishi kufananishwa na kutambulika na nchi mbalimbali Zanzibar, Mozambique, Somalia, Madagascar na baadhi ya mambo kutoka Congo na hata Cameroon. Watoto wake wanaendelea na utajiri wa muziki waliourithi kutoka kwa baba yao na utaendelea si kwa vizazi tu bali utavuka bahari, visiwa na watu.

www.groovelele.fr

**Albam**:
Dan kèr Lélé (1998); Trans-Mission (2008); Zembrocal Musical (2010)

Shukran kwa Région Réunion

---

## JAGWA MUSIC (Tanzania)

**Ijumaa 11, saa 6:15 usiku Old Fort**
**Mtindo**: coastal, roots, urban

Jagwa Music iliibuka mnamo mwaka 1992. Kama kikundi kilichotokea katika kundi maarufu la chakacha ambalo lilijulikana zaidi kwa umaarufu wa kupiga. Mziki maharusini kwa uzoefu wa miaka mingi. Mziki wa Jagwa Music ulifanyikiwa kuunda aina mpya ya Mziki maarufu kwa jina la Mchiriku. Nyimbo za Jagwa hutoa maoni kuhusu maisha ya kila siku ya Mtanzania baadhi ya maneno ya nyimbo zao yamepata umaarufu na kutolea mfano na hata kutumika na wananchi kama semi za mitaani za kila siku kwa mfano nyimbo iliopendwa na wengi kama “Maisha Popote” lakini pamoja na hayo yote bado vyombo vya habari vya Tanzania havitaki kuutambua Mziki wa Jagwa Music na Mchriku. Ni kawaida kutousikia Mziki huu kupigwa maredioni kwani Mziki huu unachukuliwa kuwa na hulka za kihuni nani mziki wa Miaka ya 1990. Mchriku ulipigwa marufuku mara kadha na vyombo vya dola, pamoja na yote hayo Mchriku unaendelea kupendwa na wengi. Ushahidi ni jinsi semi zake zinavyotumiwa kama wito na maneno yatumikayo kuvumisha biashara ya Mabasi, Madaladala na Mataxi. Jagwa Music wamesharekodi kaseti zaidi ya dozen na

wanaendelea kutoa burudani katika vitongoji vya jiji la Dar es Salaam ingawa ni mara chache kukodishwa na mahotel na mabaa hata hivyo wamefanyikiwa kuteka roho za mashabiki wake.

Kaseti:
Tulia Mke Wangu (1998), Bai Bai Abiola (1998), Mauaji Ya Kinyama(1999), Liwalo Na Liwe (2000), Tumechoka Hoi (2000), Jela Haina Mwenyewe (2001), Shughuli Gharama (2002)

---

## JAHAZI MODERN TAARAB (Tanzania)

**Jumatano 9, 5:45 usiku Old Fort**
**Mtindo**: band, fusion, taarab

Historia ya mafanikio ya Jahazi Modern Taarab ni kama kikundi kinachoongoza kwa taarab Tanzania hasa inachangiwa na sifa ya Mzee Yussuf, meneja na mmiliki wa bendi na vilevile ni mwanzilishi wa taarab ya kisasa. “Kwa kuepuka kutokufahamika tumeamua kuandika nyimbo ambazo zinalezea maisha yakimapenzi, kama kuunganisha uhusiano ambao umevunjika na kuuimarisha”anaelezea Mzee Yussuf aina yao ya muziki haikuzi chuki.

**Albam**:
2 in 1 (2006); Kazi ya Mungu Haiingiliwi (2007); Tupendane Wabaya Waulizane (2007)

---

## KWANI EXPERIENCE (South Africa)

**Ijumaa 11, saa 4:15 usiku Old Fort**
**Mtindo**: fusion, hiphop, jazz, urban

Kwani Experience ni kundi la watu sita wanamuziki wa kizazi kipya (hiphop-jazz) kutoka South Africa katika mji wa Johannesburg. Ni bend yenye makali tofauti na huu ni mfumo wa tabia yao, ujumbe wao, mwonekano wao na sauti zao. Midundo motomoto, aina tofauti za muziki kama (funk ,rap, acid, jazz, soul, African indigenous na afro pop). Yote haya yanakuja kwa staili ya kuvutia kabisa.

www.myspace.com/kwaniexp

**Albam**:
The Birth of the Mudaland Funk (2005); Live After Birth (2009)

Shukran kwa 1Time

---

## LELELELE AFRICA (Kenya)

**Jumamosi 12, saa 1:00 usiku Old Fort**
**Mtindo**: coastal, pop, taarab

Kundi la taarabu kutoka Mombasa formally known as Diamond Star lilianzishwa mnamo mwaka 1995. Kundi hili lipo makini katika uhifadhi wa lugha ya Kiswahili katika mwambao wa Afrika Mashariki. Kundi hili la wana sanaa saba hutumia ala kama harmonium, violins, tamborin na viombo vya kisasa kama vile magitaa ya umeme na vinanda pamoja na sauti za waimbaji. Lelelele Africa kweli inawakilisha utajiri mkubwa wa mziki wa taarabu ndani ya Kenya. Hivi sasa kikundi hiki kinashugulikia kurekodi kazi zake za zamani katika wadhifu wa digital na utenegenezaji wa video zao ambazo zilirekodiwa kitambo katika mfumo wa redio na kassetti. Sasa wanaendelea na uhifadhi wa tungo za Elchie ambazo zingepotea pasipo kurekodiwa na kuhifadhiwa uzuri.

**Albam**:
Mombasa Michikicho and Lololo (2010)

## LES FRÈRES SISSOKO (Senegal)

**Jumatano 9, saa 11:55 jioni Old Fort**
**Alhamisi 10, saa 11:55 jioni Old Fort**
**Mtindo**: acoustic, roots, traditional

Bao na Sadio Sissoko walizaliwa toka katika familia ya wanamziki "wakongwe" wa huko Senegali wanamziki hawa wawili walianza kupiga chombo cha kisenegali kijulanacho kama kora tangu wakiwa na umri mdogo wa miaka saba pamoja na hilo. Wanamziki hawa vilevile ni wajuzi wa upigaji magitaa, ngoma, violini na saxophone. Kwa sasa wanaishi nchini Ubeligiji. Les Freres Sissoko kama bendi huchanganya mziki wa asili wakisenegali ambao unatokea katika kabila la Mandingo mchakato huo wakimziki ni kutoka mtindo kama Reggae, Jazz, Zouk na Salsa. Pamoja na kwamba Mziki wao una msukumo mkubwa kutoka katika utamaduni wakisenegali vyombo vya kisasa wanavyovitumia vimeongezea vionjo vya aina yake. Huku wakiongezea nguvu na Komlan Octave katika ngoma na Wouter Van den Abeele apigae violin wanaziki hawa wanne pamoja wanatarajia kutoka burdani yakipekee wafikapo Zanzibar.

Shukran kwa Communaute Française Wallonie-Bruxelles

---

## MLIMANI PARK ORCHESTRA (Tanzania)

**Alhamisi 10, saa 6:20 usiku Old Fort**

**Mtindo**: band, rumba

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1978 takriban miaka 36 iliopita Mlimani Park inabaki kuwa bendi maarufu nchini Tanzania kutokana nakua na vibao vingi maarufu utunzi wa Magwiji wa Mziki kama Bitchuka, Muhiddin Maalim, Gurumo, Cosmos Chidumule na Shaaban Debe. Mlimani Park ni maarufu kwa hoja zao za kimziki zilizoundwa vyema kwa mashairi mazuri ambazo huimbwa na safu yao ya waiimbaji. Ingawa ni hulka ya wanamziki wa kitanzania kuandika nyimbo nzuri lakini pamoja na hayo Mlimani Park (wana Sikinde) ni wakali wa matumizi ya vyombo vya Mziki. Mziki wa Mlimani Park unapo sikika na safu nzima ya wapuliza Matarumbeta ni burudani tosha, hii ikiwa ni sababu mmoja wapo ya kukubalika kwao na vilevile ni chapa bidhaa yao inayowapa sifa. Onyesho la Mlimani Park huufika kilele majira ya saa sita usiku hapo ndipo mchemko unaanza kwani safu ya magita ya solo huanza kujibishana na wakati gitaa la bass linaongezea mwendo wa mziki na kufanyakazi vizuri na wacheza shoo wao zaidi uchezaji shoo. Mziki wa Sikinde unatohoa mitindo asilia mbalimbali kutoka katika ngoma ya asili ya mdundiko. Mara nyingi watazamaji hutengenza gwaride ambalo hujumuisha hadi wanamziki wakiwa kazini stejini.

---

## MOHAMED ILYAS NA NYOTA ZA ZAMEREMETA (Zanzibar)

**Jumatano 9, saa 1:00 usiku Old Fort**

**Mtindo**: pop, taarab, traditional

Mwanamuziki huyu anatokea mila na desturi ya waimbaji taarabu waliochukua uhalisi wa sanaa ya kiaarabu na kufanyikiwa kuigeuza sanaa hii kua ya kizanzibari. Anasimama kidete katika utamaduni huu wa kimuziki huku akiichanganya mvuto na maongozo ya mufatano wa sauti za kimuziki kutoka Ulaya. Mohamed Ilyas alianza kazi za muziki akiwa mpulizaji wa ala ya nai na vilevile kiongozi katika safu ya waimbaji katika kundi gwiji la Taarabu visiwani Unguja Nadi Ikwani Safaa kwa miaka mingi. Alifanya utunzi wake wa mwanzo akiwa na miaka 14. Analipofisha miaka 18 alianza kujifunza kupiga ala ya accordion na kinanda. Pindi alifariki mwalimu wake marehemu Seif Salim mwaka 2000 Mohamed aliamua kuanza upigaji wa ala ya violin. Mwaka 1988 alirekodi akiwa na GlobeStyle Records ya London Uiingereza akiwa na Nadi Ikwani Safaa, aliposhiriki kama mpiga violin na mwimbaji. Utokaji wake kama mwanamuziki solo na bendi yake Nyota Zameremeta ulikuja rasmi pindi alipofuzu mafunzo ya uimbaji na kwa miaka miwili Cologne nchini Ujerumani. Hii ililetwa kutokana uendelezaji wa kipaji chake kama mwanamuziki binafsi na kiongozi wa Nyota Zameremeta. Kundi hilo limepitia njia zote zenye mafanyikio ya juu na hali ngumu kama kikundi

binafsi hapa Unguja ni kundi lililotukuka kwa uhifadhi wa utamaduni na kutambulika. Kundi hili limeshafanya ziara nyingi za kimataifa, ni sharti katika ratiba za utamaduni Zanzibar. Mafanyikio ya hivi karibuni yalitokae mwaka 2009 baada ya kufyatua album yao *Taarab* iliouza mamia ya nakala ulmwenguni kote. Mwaka huu kundi hili litamshrikisha gwiji wa taarab Bi Kidude stegini.

**Albam**:
Taarab (2009)

---

## MUTHONI THE DRUMMER QUEEN (Kenya)

**Jumamosi 12, saa 4:00 usiku Old Fort**
**Mtindo**: floetry, fusion, roots, urban

Mwanadada mtunzi na muimbaji mwanamashairi mpiga ngoma na mwanaharakati wa maswala ya kijamii Muthoni Ndonga alizaliwa na kukulia Nairobi nchini Kenya. Tayari keshafikiriwa kuwa nafasi ta uongozi katika anga za burudani na maswala ya kijamii Muziki wa Muthoni ni wa kibunifu ambao unachanganya mfuatano wa sauti za kimuziki na mwendo wakimuziki za kiafrika kwakutumia mifano ya kila siku ya jamii za kiafrikakwa kutumia lugha za kiingerenza, kikuyu na Kiswahili. Muthoni vilevile huchanganya mitindo mbalmbali katika muziki wake ikiwemo salsa kwaito, afrorock taarab,rap naR&B huu ni mseto wa kimuziki  inspired na mapenzi,mahusiano ya ndoa siasa na maswala ya kiroho wito wa mwanadada katika utunzi wake ni kazi yenye wito hope curiosty and courage na nguvu mseto wamuziki wake  una blend tamaduni za kiafrika mashariki  na tamaduni za vijana wa kizazi kipya.

www.penyafrica.com

**Albam**:
Mambo Bado (2008); The Human Condition (2010)

Shukran kwa Fly540

---

## ORCHESTRE POLY RYTHMO DE COTONOU (Benin)

**Alhamisi 10, 4:15 usiku Old Fort**
**Jumamosi 12, 5:00 usiku Old Fort**
**Mtindo**: afrobeat, roots, fusion

Kundi la Le Tout Puissant Orchestre Poly Rythmo De Cotonou ni moja siri kubwa iliyojificha ndani ya Afrika Magharibi. Kundi hili Gwiji la Muziki limeshafanya maonyesho na magwiji wa muziki Afrika kama vile Fela Kuti, Miriam Makeba, Manu Dibango na Orquesta Aragon. Mnamo mwaka 1969 ikitumia chanzo cha muziki wenye midundo ya kimuziki ya ngoma asilia ya sherehe za *Vodoun* kutoka nchini Benin. Ochestre Poly Rythmo iliundwa, kama vile haitoshi wana Poly Rythmo waliongezea vionjo muziki wao kwa kuuchanganya muziki wao na wakali wa miaka hiyo kama vile Johnny Hallyday ,Dalida na James Brown. Mchanganyiko huo wakibunifu uliunda aina ya muziki ya kipekee ulioiwezesha bendi kupokea heshima kubwa katika anga yakimuziki na kukubalika sana Afrika Magharibi kote. Hadi hii leo wamesharekodi zaidi ya nyimbo 500 vikiwemo vibao vyao vikali kama ‘Gbeti Madiro’ na ‘Mille Fois Merci’.

“Tumeshafanya kazi mara nyingi tu na Fela Kuti kila alipofanya maonyesho yake Cotonou [mji Mkuu wa Benin] na mara nyingi tulikutana naye EMI Studio Lagos nchini Nigeria”alisema Clement mmoja wa viongozi wa Poly Rythmo. Mpaka kufikia mwaka 1980 bendi hii ilifanyikiwa kufanya maonyesho katika nchi mbalimbali barani Afrika kama vile Niger, Togo, Nigeria, Burkina Faso, Angola na Cote d’Ivoire. Lakini kutokana machafuko ya kisiasa na kuyumba kwa uchumi nchini Benin na vilevile kufariki kwa mpiga gitaa wao mashuhuri Bw Bernard Papillion Zoundegnon na Bw Yehousi Leopold ilifikirika kwamba kutokana na matatizo hayo ingekua ndio mwisho bendi hii. Lakini takribani miaka arobaini sasa tangu kuanzishwa kwa kundi hili, Orchestre Poly Rhytmo wapo tayari kabisa kukuletea burudani kwa mara ya kwanza ndani ya Africa Mashariki, wakiwa njiani kuelekea katika ziara yao ya kwanza yakimuziki nje ya bara la Afrika kuelekea nchi za Ulaya wakipitia Zanzibar.

## OTENTIKK STREET BROTHERS (Mauritius)

**Ijumaa 11, saa 5:20 usiku Old Fort**
**Jumamosi 12, saa 6:15 usiku Old Fort**
**Mtindo**: reggae, roots, urban

Historia ya kundi la Mauritian Reggae Creole, Otentikk Street Brothers ilianza mwaka 1992. Wakati wakiwa kwenye mitaa ya *hometown* kama vijana wengine wengi ulimwenguni. Bruno na Koeny ni ndugu waathirika na virusi vya kimuziki vya hiphop ambavyo vinasambazwa na wakali kama Public Enemy, Run DMC, LL Cool J. Baada ya miaka kadhaa safu yao ya wafokaji ilibadilika nakuchukuliwa na Blakkayo msanii mgeni kipindi hicho ambae ni mkali wa mistari. Tikkenzo na Dagger killa walifuata kuongezea nguvu kundi hili mistari inayopendwa imetokea kupendwa na wengi. Otentikk Street Brothers aka OSB Crew wamekua kundi la kutambulika ndani ya nchi za Ukanda wa Bahari ya Hindi. Mwaka 2004 walitoa albam yao mpya iitwayo *Rewey Twa* pamoja na kwamba nyimbo karibu zote kwenye albam yao zipo kwenye maadhi ya Reggae na Dancehall lakini muziki wao umekuwa ni tofauti na Reggae zilizotengenezwa Ulaya na Jamaik. Uwezo wao wakuiongoza na *séga,* ngoma ya kimauritius, ndio inawafanya kusikilia nafasi walio nayo.

www.myspace.com/osbcrewms

**Albam**:
Ragga Kreol (1994); Expresyon Libere (1997); Nou Kkila (2001); Revey Twa (2004); Revey Twa European Edition (2007)

Shukran kwa Wizara ya Sanaa na Utamaduni, Mauritius

---

## PERCUSSION DISCUSSION AFRIKA (Uganda)

**Jumatano 9, saa 4:45 usiku Old Fort**

**Mtindo**: fusion, traditional, roots

Percussion Discussion Afrika sasa ni kundi imara na mstari wa mbele katika Mziki wa Uganda. Hii imesababishwa kwa kufanikiwa kuchanganya vifaa vya kisasa na vya asili tangu mwaka 1997. Mwimbo wao '*Nawakunde' ilitumiwa* kwenye sound track ya filamu ya block buster 'Last king of Scotland', ilitolewa mwaka 2006. Na kuwa miongoni mwa mabalozi wa utamaduni wa Uganda, Percussion Discussion Afrika wanakuza utajiri wa mziki na mashairi wa Uganda. Kupendezesha jukwaa na muonekano wawapo jukwaani, wasikilizaji na onyesho lao hua halisahauliki.

www.pdasewi.net

---

## SOUSOU & MAHER CISSOKO (Senegal / Sweden)

**Jumamosi 12, 11:55 usiku Old Fort**
**Mtindo**: band, jazz, roots, traditional

Wanamziki hawa wawili wanatambulika kuwa uimbaji wao uliojawa maelezo na mwendo mziki wakitofauti. Na si kama bendi nyingine Sousou na Maher wanakuletea mziki wenye ladha ya Afrika Magharibi tangu kuifungua Albam yao 2008, inaitwa *Adouna*. Wameshafanya maonyesho mbalimbali katika nchi za Scandinavia, Senegali na Afrika Kusini. Maher Cissoko ametokea katika familia ya wanamziki wakongwe na kurithishwa ala hii ya kora kutoka kwa wazee wake. Mwanadada Sousou Cissoko ni mwanamziki wa kipekee wa kike anaeshikilia rekodi hiyo mpaka leo. Bendi hii inajumuisha wasanii kutoka nchi kama Senegali na Sweden ambao niwapigaji wa magitaa, percussion na bass.

www.sousoumaher.com; www.ajabu.com

**Albam**: Adouna (2008)

Shukran kwa Baraza la Sanaa la Sweden

## SUKIAFRICA SUKIYAKI ALLSTARS (Various)

**Alhamisi 10, saa 1:00 usiku Old Fort**
**Mtindo**: band, fusion

Ni mastaa watatu kutoka Afrika na vingozi wa mziki wa kiasia wamebadilisha na kuunganisha ubunifu wao na kufanya maonyesho, uimbaji, uchezaji vile vile kutengeneza uhusiano wa kimuziki kati ya mabara yetu mawili Afrika na Asia. Kuzaliwa kwake kulitokana na tamasha linalojulikana kama "Sukiyaki meets the World". Sukiyaki ni mjumuisho maalum wa muimbaji na mchezaji mbira Chiwoniso kutoka Zimbabwe, piga gita Peter Solo kutoka Togo, Erik Aliana kutoka Cameroon, muimbaji na mpiga marimba Sakaki Mango, Chang Jaehyo kutoka Korea na mpiga Tumba Ndana kutoka Japan. Mwonekano wao Sauti za Busara 2011 ni mafanikio ya Sukiyaki Sukiafrica Afrika tour ambapo itaonyeshwa maonyesho ya moja kwa moja(live) kama zilivyopigwa Zimbabwe, South Africa na Swaziland.

www.sukiyaki.cc/artists/index.html

**Albam**:
**Chiwoniso**: Ancient Voices (2003), Timeless (2006), Rebel Women (2009)
**Peter Solo**: Miadome (2006)
**Erik Aliana**: Just Africa (2005)
**Chang Jaehyo**: Barame Soop (2008)
**Sakaki Mango**: Limba Train (2006), Limba Rock (2008)
**Ndana**: Sound of Africa (2006), Inochi no Uta (2009)

Shukran kwa Japan Foundation

---

## YAABA FUNK (UK)

**Jumapili 13, saa 5:20 usiku Old Fort**
**Mtindo**: afrobeat, band

Wanaeleweka kuchana majukwaa kumbi za starehe kwa staili yao ya Mziki wenye nguvu mchanganyiko wa afro funk beats nchini Uingereza. Ni wanamuziki kutoka Uingereza kitongoji cha Brixton London kusini, wanachama wote wa bendi hii walikutana London miaka ya tisini. Ni katika mandhari ya ngoma za kiafika nchini Uingereza ambapo wapigaji wakiaafrika hukusanyika na ndipo Yaaba funk walikutana na kuaanza kufanya mazoezi pamoja. Kundi lilianzishwa rasmi mwaka 2006 likiwa na wanachama marafiki kutoka Ghana, Marekani, Martinique, Jamaica Italy na Germany. Uanzilishi wa kundi hili ndio ulianzisha aina mpya ya Mziki ujulikanayo kama Punky Afro Roots ya karne ya 21!

www.yaabafunk.com

**Albam**:
Afrobeast (2010)

Shukran kwa PRS na British Council

# Wasanii wengine ambao watapanda jukwaa la Sauti za Busara 2011, wafuatao:

**Bi Kidude,** bibi yetu hapa Zanzibar!
Pamoja na Mohamed Ilyas na Nyota Zameremeta: Jumatano 9, saa 1:00 usiku Old Fort
Pamoja na Culture Musical Club: Ijumaa 11, saa 1:00 usiku Old Fort

**Black Roots**, mchanganyiko wa muziki na ngoma za asili na kisasa kutoka Zanzibar
Alhamsi 10, saa 2:20 usiku Old Fort

**Cross Border**, muziki wa mduara na mchanganyiko
Ijumaa 11, saa 10:30 jioni Old Fort

**Maulidi ya Homu ya Mtendeni**
Jumatano 9, saa 3:10 usiku Old Fort

**NEWS Quartet** mchanganyiko wa muziki kutoka Mauritainia, Norway na Zanzibar
Ijumaa 11, 12:05 jioni Old Fort

**Nomakanjani Arts** ngoma na uchezaji wa asili kutoka Zambia
Jumapili 3, 1:00 usiku Old Fort

**Nyota Kali Band,** sarakasi na ngoma za asili kutoka Dar es Salaam
Jumamosi 12, 11:00 jioni Old Fort

**Sauda**, mwimbaji wa jazz na mchanganyiko wa asili wa Tanzania
Alhamisi 10, 11:00 jioni Old Fort

**Tunaweza Band**, muziki wa dansi na wa asili kutoka Dar es Salaam
Jumatano 9, 11:00 jioni Old Fort

**Sinachuki Kidumbak** (Zanzibar)
Alhamisi 10, 5:25 usiku Old Fort

**Staff Band Namasabo**, muziki wa asili kutoka Ukerewe, Mwanza
Jumapili 13, 11:55 jioni Old Fort

**Vusa Mkhaya & Band**, mchanganyiko wa muziki wa Zimbabwe na Ulaya
Jumapili 13, saa 11:00 jioni Old Fort

**Wanyambukwa Arts Group**, muziki wa asili wa kabila la Wagogo
Jumatano 9, saa 2:20 usiku Old Fort

**Kwa maelezo zaidi kuhusu vikundi vyote tafadhali utembelee tovuti ya [www.busaramusic.org](http://www.busaramusic.org)**